TAFSIRI ORIJINO YA TOLEO LA MWAKA 1937

# FIKIRI NA UTAJIRIKE

# THINK AND GROW RICH

SWAHILI EDITION

## NAPOLEON HILL

Translated by Peter A. Tarimo

# FIKIRI NA UTAJIRIKE

# THINK AND GROW RICH

SWAHILI- EDITION

NAPOLEON HILL

*Translated by Peter A. Tarimo*

FIKIRI NA UTAJIRIKE
(THINK & GROW RICH – SWAHILI EDITION)

Copyright © 2021 Peter Augustino Tarimo

Haki zote zimehifadhiwa chini ya sheria ya Tanzania na zile za Kimataifa. Hairuhusiwi kunakili, kudurufu au kutumia sehemu ya tafsiri ya kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili kwa njia yeyote ile bila idhini ya mfasiri(mmiliki). Kufanya hivyo ni kosa kisheria linaloweza kusababisha mashtaka dhidi yako toka kwa waandaaji wa tafsiri hii.

ISBN: 978-9976-88-937-6

Wakati kitabu asilia cha Think and Grow Rich katika lugha ya kiingereza sasa hivi ni mali ya umma(Public domain), tafsiri yake hii kwa Kiswahili bado ni mali ya mfasiri na waandaaji wake. Tafsiri hii imetokana na kazi ya asili ya Napoleon Hill ya mwaka 1937 iliyochapishwa chini ya *The Ralston Society*.

Tafsiri hii pia inaweza katika baadhi ya sehemu au maneno ikapotosha maana ya asili lakini waandaaji tumefanya kila jitihada kuhakikisha kitabu kinabeba maana ileile aliyokusudia Napoleo Hill mwenyewe.

Hivyo hatutabeba dhamana yeyote kutokana na upotofu ama hasara inayoweza kutokea baada ya mtu kusoma tafsiri ya kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili.

Kitabu na Jalada vimesanifiwa na *Self Help Books Tanzania*

Mawasiliano:
Peter Augustino Tarimo
Simu: 0765553030 / 0712202244
Baruapepe: jifunzeujasiriamali@gmail.com
**www.jifunzeujasiriamali.co.tz**

# WAKFU

*Tafsiri kwa kiswahili ya kitabu hiki cha THINK & GROW RICH ni kwa ajili ya watu wote wa Tanzania na Ukanda mzima wa Afrika ya Mashariki na Kati wanaozungumza Kiswahili, masikini wanaotaabika katika lindi la ukosefu mkubwa wa maarifa sahihi ya jinsi akili zao zinavyofanya kazi, walio na uwezo mkubwa pasipo wao wenyewe kujua. Kukosa huko maarifa kunasababisha wengi kuendelea kufungwa na minyororo ya umasikini, maradhi, imani za kishirikina na imani nyinginezo potofu zisizokuwa na faida yeyote ile bali Taabu tu na Mashaka.*

# YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| | SHUKRANI | i |
| Sura ya 1 | UTANGULIZI | 17 |
| Sura ya 2 | SHAUKU | 43 |
| Sura ya 3 | IMANI | 75 |
| Sura ya 4 | KUJISHAURI-BINAFSI | 107 |
| Sura ya 5 | UJUZI MAALUMU | 117 |
| Sura ya 6 | UBUNIFU | 141 |
| Sura ya 7 | MIPANGO ILIYORATIBIWA | 163 |
| Sura ya 8 | MAAMUZI | 219 |
| Sura ya 9 | MSIMAMO | 237 |
| Sura ya 10 | NGUVU YA USHIRIKA | 263 |
| Sura ya 11 | MAAJABU YA KUGEUZA FIKRA ZA KIMAPENZI | 275 |
| Sura ya 12 | AKILI YA NDANI | 311 |
| Sura ya 13 | UBONGO | 323 |
| Sura ya 14 | MLANGO-FAHAMU WA 6 | 335 |
| Sura ya 15 | JINSI YA KUSHINDA MIZIMU 6 YA HOFU | 353 |

# SHUKRANI

KATIKA kazi ya kukitafsiri kitabu hiki napenda kutoa shukrani zangu za dhati kama ifuatavyo, Kwanza kabisa ni kwa **MWENYEZI MUNGU** aliyeumba vitu vyote ambaye katika kitabu hiki Napoleo Hill kukwepa upande wa dini yeyote ile amemtaja kama NGUVU KUU ISIYO NA MIPAKA(INFINITE INTELLIGENCE).

Pili ni kwa Mwandishi mwenyewe **Bwana Napoleon Hill** pamoja na **Andrew Carnegie**, tajiri aliyeasisi wazo hili akilini mwake. Kukosa wao leo hii nisingelikuwa natafsiri kitabu hiki. MUNGU awarehemu.

Tatu ni kwa Familia yangu, wapendwa Baba na Mama, Mke na watoto wangu kwa kuvumilia kunikosa muda wote nafanya kazi hii.

Nne ni kwa Waandishi wa vitabu walionivutia na kunihamasisha, kipekee zaidi Watanzania wawili waishio Marekani lakini walio na uzalendo mkubwa kwa nchi yao ya Tanzania. Siyo mimi tu, wamewahamasisha pia maelfu ya vijana wengine wa Kitanzania kwenye tasnia hii ya uandishi vitabu kupitia kazi zao mtandaoni. Nao ni hawa hapa;

**Profesa Joseph Mbele**: Msomi huyu ni mtu wa ajabu sana kwenye tasnia ya vitabu kwa jinsi anavyopenda kusoma, hununua karibu kila kitabu kinachotungwa na Mtanzania mwenzake akijua kinafaa, nina deni kwake la kitabu alichonilipa fedha akiwa Marekani pasipo mimi kumtumia kitabu aliponiagiza kumpelekea mtu mmoja aishie Sinza lakini nikamkuta amelazwa hospitalini nikashindwa kumpatia kitabu siku hiyo, baadae vitabu viliisha na hadi hivi leo sijamlipa kitabu.

Mara yangu ya kwanza kujua mtu unaweza kutunga kitabu na kukiweka Amazon au Lulu bure nilijua kupitia maandishi yake blog ya ***"Hapa Kwetu"*** zaidi ya miaka 10 iliyopita, nikahamasika kutafsiri kitabu hiki kwani nilifahamu nitapomaliza nitakichapisha bila gharama huko. Profesa Mbele Ametunga vitabu vingi vizuri kikiwamo kile cha *Africans and Americans Embracing Cultural Differences* na *Matengo Folktales*

Mzalendo wa pili ni **Bwana Ernest B. Makulilo** aishie pia Marekani, yeye kupitia kozi na video zake You Tube niliweza hatimaye kukiweka kitabu hiki katika mtandao wa Amazon japo katika hatua za mwisho '*walizingua'* lugha ikashindikana kukichapisha, napenda vitabu vyake cha A *Loving Father* na *Clare The Happiest* Girl. Ametunga pia vitabu vingine vingi kikiwemo *Albino Killings in Tanzania: Witchcraft and Racism?*

Nimewataja wazalendo hawa makusudi, kuelezea jinsi maadili ya Kimarekani ya moyo wa kuwatakia wengine fursa na mafanikio yalivyo na nguvu na matokeo chanya kwa jamii, maadili ambayo pia ndiyo yanayotawala kwa kiasi kikubwa katika kitabu hiki. Ni katika nchi ya Marekani pekee duniani mtu kutoka dunia ya tatu unaweza ukaweka malengo ya mjukuu au mtoto wako kuja kuwa Rais wa Marekani na kweli ikaja kuwa hivyo .

Si kama nawasifia sana Wamarekani au Mungu amewabariki zaidi kuliko Mataifa mengine, la hasha! bali ni kutokana na wengi wao kuikumbatia **FALSAFA** iliyo ndani ya kitabu hiki kwamba; "***BINADAMU ANAO UWEZO WA KUWA AU KUFANYA KITU CHOCHOTE KILE AMBACHO AKILI YAKE INA UWEZO WA KUKIFIKIRIA."***

Mtu kutoka Taifa jingine lolote lile duniani, aliye na rangi, dini, au jinsia yeyote anaweza pia kufanya vilevile sawa na Wamarekani ikiwa tu naye atakumbatia falsafa hiyo. Wivu, Chuki, Ubaguzi, Uchoyo na Visasi kamwe havina nafasi kwa watu waliofunguliwa na falsafa inayopatikana ndani ya kitabu hiki.

# DIBAJI YA MWANDISHI

KILA SURA YA KITABU hiki imetaja siri ya kupata pesa ambayo imetoa bahati kwa zaidi ya watu 500 matajiri zaidi ambao niliwachunguza kwa makini katika muda wa kipindi kirefu.

Siri yenyewe nilijulishwa na mtu aliyejulikana kama Andrew Carnegie zaidi ya robo karne iliyopita. Akiwa ni mzee wa Kiskoti, mwerevu, na aliyependwa na watu, bila ya kujali aliitumbukiza siri hiyo ndani ya akili yangu ningali bado kijana mdogo. Kisha aliketi katika kiti chake, huku macho yake yakimetameta kwa furaha, alitazama kwa makini kuona kama nilikuwa na akili za kutosha kutambua umuhimu wa kile alichokuwa amenieleza.

Alipoona sasa nilikuwa nimekwishapata lile wazo, aliniuliza ikiwa kama ningekuwa tayari kupoteza miaka 20 au zaidi nikijitayarisha mwenyewe katika kwenda kulieneza duniani kote kwa wanaume na wanawake ambao pasipo siri hii wasingeweza kupiga hatua yeyote ile ya maana kimaisha. Nilisema, ningeweza na kwa ushirikiano wa Bwana Carnegie, nimeweza kutimiza ahadi yangu.

Kitabu hiki kimebeba siri ambayo imekuwa ikijaribiwa kivitendo na maelfu ya watu kutoka karibu kila nyanja ya maisha. Lilikuwa ni wazo la Bwana Carnegie, kanuni ya ajabu, iliyompa utajiri mkubwa na iliyopaswa kufikishwa kwa watu wasiokuwa na muda wa kuchunguza ni jinsi gani watu wanaweza kutajirika.

Alitumaini kwamba ningeweza kufanya majaribio na kuonyesha utimilifu wa kanuni yenyewe kwa kupitia uzoefu wa wanaume na wanawake katika kila nyanja. Aliamini kwamba kanuni hii ingepaswa kufundishwa katika shule zote na vyuo, na alitoa maoni yake kwamba, ikiwa kama ingefundishwa sawasawa, ingeweza kuleta mapinduzi katika mfumo mzima wa elimu ambapo muda wa mwanafunzi kukaa shuleni ungeweza kupunguzwa kwa zaidi ya nusu.

Uzoefu wake na Charles M. Schwab na vijana wengine wa aina ya Bwana Schwab, walimshawishi Bwana Carnegie kwamba mengi ya yale yaliyokuwa yakifundishwa mashuleni hayakuwa na thamani yeyote ukiyalinganisha na biashara ya kujikimu kimaisha au kujichumia utajiri. Alifikia uamuzi huu

baada ya kuwaweka katika biashara zake kijana mmoja baada ya mwingine, wengi wao wakiwa na kiwango kidogo cha elimu, aliwajengea ndani mwao uwezo adimu wa uongozi kwa kuwafundisha namna ya kuitumia kanuni hii. Hatimaye mafunzo yake yalimfanya kila aliyeyafuata kupata mafanikio.

Kwenye sura inayohusu Imani, utasoma habari ya kushangaza ya namna kanuni hii ilivyotumiwa na shirika moja kubwa la chuma cha pua Marekani, United States Steel Corporation. Ilichukuliwa na kufanyiwa kazi na mmoja wa vijana ambaye Bwana Carnegie alithibitisha kwamba kanuni yake itafanya kazi kwa wale wote waliokuwa tayari kuipokea. Matumizi ya siri hii kwa mara moja yaliyofanywa na kijana Charles M. Schwab yalimletea mafanikio makubwa kifedha na pia *kifursa.* Kwa kukadiria harakaharaka, matumizi haya ya siri yalikuwa na thamani ipatayo dola million 600.

Ukweli huu - na ni ukweli unaojulikana vizuri kwa wale wote waliomfahamu Bwana Carnegie, unakupa picha halisi ya kile utakachokipata baada ya kukisoma kitabu hiki, ilimradi tu *unakifahamu kile unachokitaka.*

Hata kabla ya kufanyiwa majaribio kivitendo kwa muda wa miaka 20, siri hii ilikwisha tumiwa na watu zaidi ya 100,000 wanaume kwa wanawake ambao waliitumia kwa faida zao binafsi kwa namna ile ile kama Bwana Carnegie alivyoeleza. Baadhi yao wamepata nayo mafanikio, wengine wameitumia kwa mafanikio katika kuleta utulivu majumbani

mwao. Mchungaji mmoja aliitumia kwa ufanisi kiasi kwamba ilimletea kipato cha juu cha $75,000 kwa mwaka.

Arthur Nash fundi nguo katika mji wa cincinati aliitumia biashara yake iliyokuwa karibu kufilisika kama “chombo cha majaribio” kwa ajili ya kuijaribu kanuni hii. Biashara ilirudia uhai wake na kuwapa utajiri wamiliki wake. Bado inaendelea ingawa Bwana Nash ameshatangulia. Jaribio lilikuwa ni la kipekee kiasi kwamba magazeti na majarida yalilipatia zawadi ya nafasi za matangazo yenye thamani ya zaidi ya dola milioni moja.

Niliitoa siri kwa Jennings Randolph siku aliyomaliza chuo na ameitumia kwa mafanikio kiasi kwamba sasa hivi anatumikia muhula wake wa tatu kama mjumbe wa baraza la Congress akiwa na fursa bora kabisa ya kuendelea kuitumia mpaka inampeleka ikulu ya White House.

Wakati nilipokuwa nikihudumu kama Meneja wa matangazo wa Chuo kikuuu cha La-Sale Extension, wakati jina halijakua sana nilipata bahati ya kumuona J. G. Chapline, Rais wa chuo akiitumia kanuni hii kwa ufanisi kiasi kwamba tangu hapo alikifanya chuo cha LaSalle moja kati ya vyuo vya juu vikubwa kabisa nchini.

Siri ninayoizungumzia imetajwa siyo chini ya mara mia ndani ya kitabu hiki. Haijatajwa moja kwa moja, kwani inaonekana kufanya kazi kwa ufanisi zaidi pale ambapo inaachwa pasipo kubainishwa bayana na

kuachwa wazi ambapo kwa *WALE WALIOKUWA TAYARI na KUITAFUTA*, wanaweza kuipata. Hii ndiyo sababu iliyomfanya Bwana Carnegie kuitumbukiza siri hii ndani mwangu kimya kimya namna hiyo, pasipo hata kunitajia jina kamili la siri yenyewe.

Ikiwa upo *TAYARI* kuitumia siri yenyewe, utaigundua angalao mara moja katika kila sura ya kitabu hiki. Natamani ningeweza kukueleza ni jinsi gani utakavyofahamu ikiwa umekuwa tayari, lakini hilo laweza kukunyima nyingi ya faida ambazo utaweza kuzipata endapo utagundua mwenyewe kivyako.

Wakati kitabu hiki kilipokuwa kikiandikwa, kijana wangu mwenyewe ambaye alikuwa akimalizia mwaka wake wa mwisho chuoni, alichukua mswada wa kitabu sura ya 2 akausoma na kujigundulia siri mwenyewe. Alizitumia zile taarifa kwa ufanisi mkubwa, kiasi kwamba alipata moja kwa moja kazi kwa mshahara wa kuanzia mkubwa kupita hata wale waliolingana nae. Habari zake kwa ufupi zimeelezwa katika sura ya 2.

Utakapoisoma pengine utatupilia mbali fikra zozote unazowezakuwa ulikuwa nazo pindi utakapoanza kukisoma kitabu mwanzoni kutokana na sababu kwamba kinaahidi mambo mengi sana. Na vile vile, ikiwa umewahi kukatishwa tamaa, umewahi kuwa na matatizo makubwa yaliyoshindikana, ikiwa uliwahi kujaribiwa ukashindwa, ikiwa uliwahi kupata ulemavu kutokana na ugonjwa ama ajali, habari hii juu ya mtoto wangu aliyegundua na kutumia kanuni ya Carnegie inaweza ikathibitika kuwa chemichemi ndani

ya jangwa la matumaini yaliyopotea ambayo umekuwa ukiisaka.

Siri hii ilitumika kwa kiasi kikubwa na Rais Woodrow Wilson wakati wa vita kuu ya 1 ya Dunia. Kila mwanajeshi aliyepigana katika vita hii, alipenyezewa siri hii kwa uangalifu mkubwa kupitia mafunzo waliyopewa kabla ya kwenda katika uwanja wa mapambano. Rais Wilson aliniambia kuwa hicho ndicho kilichokuwa kigezo kikubwa katika kukusanya fedha zilizohitajika kugharamia vita.

Mapema katika karne ya 21, Manuel L. Quezon (Aliyekuja kuwa pia Kamishna Mkuu wa visiwa vya Ufilipino) alivutiwa na siri hii katika kudai uhuru wa watu wake, hatima yake alikuja kuwa Rais wao wa kwanza.

Kitu cha kustaajabisha kuhusu siri hii ni kwamba, wale wanaoichukua na kuitumia, hujikuta wenyewe wakipata mafanikio makubwa huku wakitumia nguvu kidogo sana, na kamwe huwa hawarudi tena kwenye maanguko! Ikiwa una shaka na hili, soma majina na rekodi za wale watu walioitumia popote pale walipotajwa na mwisho utakubali.

*Hakuna kitu kama,* KUPATA KITU PASIPO KUTOA CHOCHOTE!

Siri niliyoizungumzia haiwezi kupatikana hivihivi tu bure, ingawa malipo yake ni kidogo sana ukilinganisha na thamani yake halisi. Wale ambao hawana lengo katika kuitafuta siri hii kamwe hawataweza kuipata kwa gharama yeyote ile. Haiwezi

ikapewa kwa namna yeyote ile wala haiwezi ikanunuliwa kwa pesa kwasababu huja ikiwa katika sehemu mbili. Sehemu moja tayari wanakuwa nayo moja kwa moja wale waliokuwa tayari kuipokea. Siri hufanya kazi vizuri kwa wale wote waliokuwa na utayari wa kuipokea.

Wala elimu haina chochote cha kufanya nayo. Zamani kabla hata sijazaliwa siri hii ilitumiwa na mtu mmoja aliyejulikana kama Thomas A. Edison, na aliitumia kwa werevu kiasi kwamba aliweza kuwa mvumbuzi namba moja duniani ingawa elimu yake ilikuwa ni ya miezi mitatu tu. Siri ilihamishiwa kwa mshirika wa Bwana Edison, naye akaitumia kwa ufanisi. Ingawa alikuwa akipata dola 1,200 pekee kwa mwaka lakini aliweza kujipatia utajiri mkubwa na alistaafu biashara angali bado kijana. Utakutana na habari zake mwanzoni katika sura ya 1. Habari hii itakufanya uamini kwamba hata wewe unaweza ukawa tajiri, kwamba unaweza ukawa yeyote unayetamani kuwa, kwamba fedha, umaarufu, kuthaminiwa na furaha, vinaweza kumilikiwa na yeyote aliye tayari na mwenye nia ya kuwa na neema hizi.

Nitayajuaje mambo haya? unatakiwa uwe umekwishapata jibu kabla ya kumaliza kukisoma kitabu hiki. Unaweza ukakutana nayo pale ukurasa wa kwanza kabisa, au hata katika ukurasa wa mwisho.

Nilipokuwa natekeleza jukumu la utafiti kwa muda wa miaka 20, jukumu nililolifanya kutokana na Rai ya

Bwana Carnegie. Nikiwahoji mamia ya watu maarufu, wengi wao wakikubali kwamba waliweza kupata utajiri waliokuwa nao kwa kupitia kanuni(siri) ya Carnegie. Miongoni mwa watu hao ni hawa wafuatao;

HENRY FORD
WILLIAM WRIGLEY JR
JOHN WANAMAKER
JAMES J. HILL
GEORGES S. PARKER
E.M.STATLER
HENRY L. DOHERTY
CYRUS H.K. CURTIS
GEORGE EASTMAN
THEODORE ROOSEVELT
JOHN W. DAVIS
ELBERT HUBBARD
WILBUR WRIGHT
WILLIAM JENNINGS BRYAN
DR. DMTID STARR JORDAN
J. ODGEN ARMOUR
CHARLES M. SCHWAB
HARRIS F. WILLIAMS
DR. FRANK GUNSAULUS
DANIEL WILLARD
KING GILLETTE
RALPHA A. WEEKS
JUDGE DANIEL T. WRIGHT
JOHN D ROCKEFELLER
THOMAS A. EDISON
FRANK A. VANDERLIP
F. W. WOOLWORTH
COL ROBERT A. DOLLAR

EDWARD A. FILENE
EDWIN C. BARNES
ARTHUR BRISBANE
WOODROW WILSON
WM. HOWARD TAFT
LUTHER BURBANK
EDWARD W. BOK
FRANK A.MUNSEY
ELBERT H. GARY
DR. ALEXANDER GRAHAM BELL
JOHN H. PATTERSON
JULIUS ROSENWALD
STUART AUSTIN WIER
DR. FRANK CRANE
GEORGE M. ALEXANDER
J.G.CHAPPLINE
HON. JENNINGS RANDOLPH
ARTHUR NASH
CLARENCE DARROW

Majina haya yanawakilisha baadhi tu ya mamia ya Wamarekani maarufu zaidi ambao mafanikio yao kiuchumi na hata katika nyanja nyinginezo ni ushahidi kwamba, wale wenye kuelewa na kuitumia siri ya Carnegie hufika kilele cha juu kabisa cha mafanikio. Watu wote niliopata kuwafahamu ambao wamevutika kuitumia siri hii wameweza kupata mafanikio yanayoonekana katika nyanja zao walizochagua. Sijawahi kumfahamu mtu yeyote aliyejibainisha mwenyewe kupata utajiri wowote ule wa maana pasipo kuimiliki siri hii.

Kutokana na vigezo hivyo viwili, nahitimisha kwamba, siri hii ni muhimu zaidi kama sehemu ya maarifa

yanayohitajika katika kujitambua mwenyewe kuliko kitu chochote kile mtu anachoweza kukipata kupitia kile kinachojulikana kama “Elimu”.

Kwa vyovyote vile kwani ELIMU ni nini? Hili limejibiwa kwa mapana sana. Kwa kadiri elimu inavyohusika, wengi wa watu hawa maarufu walikuwa nayo kidogo sana. John Wanamaker aliwahi kuniambia kwamba, elimu kidogo aliyokuwa nayo, aliweza kuipata mithili ya meli inavyoanza safari ikiwa majini “kwa kurusha maji juu inapoanza mwendo” Henry Ford hakuwahi kufika sekondari ya juu, achiliambali chuo. Siyo kama najaribu kupunguza thamani ya elimu bali najaribu kuelezea imani yangu ya moyoni kwamba wale wanaojifunza kikamilifu na kuitumia kanuni hii hufika kileleni, kupata utajiri na kumudu maisha yao wenyewe, hata ikiwa elimu yao ni kidogo.

Mahali fulani wakati ukisoma, siri ambayo nimekuwa nikiizungumzia itaruka kutoka kwenye ukurasa wa kitabu na kusimama dhahiri mbele yako, *lakini ikiwa tu upo tayari kuipokea*! Itakapoonekana, utaitambua tu. Haijalishi ikiwa umeziona dalili zake sura ya kwanza wala ya mwisho, simama kwa muda inapojidhihirisha na ugeuze glasi yako chini kwani tukio hili litakuwa limeweka alama katika hatua muhimu mno ya upeo wa maisha yako.

Sasa tunaingia Sura ya Kwanza iliyo na habari inayomhusu rafiki yangu mpendwa sana ambaye hakuficha kukubali kuona dalili ya maajabu, na ambaye mafanikio ya biashara zake ni ushahidi tosha kwamba aliifunika chini glasi yake. Unaposoma habari

yake na wengineo, kumbuka kwamba wanashughulika na matatizo muhimu ya kimaisha kama vile, uzoefu wa watu kwa ujumla. Matatizo yatokanayo na jitihada za mtu kujitafutia maisha, kutafuta matumaini, ujasiri, ridhiko na utulivu wa akili katika kujipatia utajiri na kufurahia uhuru wa mwili na roho.

Kumbuka pia kadiri utakavyokuwa ukisoma kitabu hiki, kinahusiana na mambo ya ukweli na wala siyo riwaya, lengo lake likiwa ni kufikisha ujumbe wa kweli uliokuwa mkuu kwa kila mtu, ukweli ambao kila aliyekuwa ***tayari***, anaweza kujifunza, siyo tu NI NINI CHA KUFANYA, BALI PIA NA JINSI YA KUKIFANYA! NA KUPOKEA KICHOCHEO KINACHOHITAJIKA ILI KUANZA.

Kama neno la mwisho la matayarisho kabla hujaianza sura ya kwanza, naomba nitoe mapendekezo machache yatakayoweza kutoa mwangaza katika kuitambua siri ya Carnegie. Nalo ni hili hapa - MAFANIKIO YOTE, UTAJIRI WOTE ULIOCHUMWA, VYOTE MWANZO WAKE NI WAZO (FIKRA)!

Ikiwa upo tayari kwa siri hii, tayari unayo nusu ya siri yenyewe, kwa hiyo utaitambua mara moja nusu ya siri iliyobakia punde tu itakapofika akilini mwako.

***NAPOLEON HILL, 1937***

.

# DIBAJI YA MFASIRI

MENGI kuhusiana na kitabu hiki yameshasemwa na Mwandishi mwenyewe Bwana Napoleon Hill, mimi hapa kazi yangu kubwa ilikuwa ni kukitafsiri tu kwa Kiswahili kitabu hiki mashuhuri zaidi Duniani cha elimu ya fedha na Mafanikio kuwahi kuandikwa, kazi ambayo niliianza karibu muongo mmoja uliopita. Kwa kweli sikuwa naandika tafsiri hii haraka kwani niliifanya kama mfululizo(series) katika blogu yangu ya ***jifunzeujasiriamali***.

Hii ni tafsiri kamili ya kitabu cha **Think and Grow Rich** neno kwa neno na wala siyo uchambuzi, hivyo unaweza kuona kwamba ni kwa jinsi gani ukikisoma unapata ladha halisi ya kitabu chenyewe iliyokusudiwa na Napoleon Hill mwaka 1937. Siwezi kukataa, ni kweli makosa au hitilafu za hapa na pale

zinaweza zikawepo lakini naamini pia miongoni mwa wasomaji watakuwepo pia wenye ujuzi mkubwa zaidi yangu na kwa pamoja tunaweza kuzirekebisha.

Wapo watu wanaobeza Kiswahili kuwa hakiwezi kushindana Kimataifa lakini niwakumbushe tu kwamba kuna kazi kubwa sana na mashuhuri Duniani zilizowahi kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ikawezekana na baadhi ya mifano yake ni hii hapa; Vitabu vya Shakespear, ***Mabepari wa Venisi na Juliasi Kaizari*** vilivyotafsiriwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Vitabu vitakatifu vya ***Quran na Biblia*** nk. Pamoja na hiki cha ***Think and Grow Rich***, huu ni ushahidi tosha kwamba Kiswahili ni tajiri na kina uwezo mkubwa sawasawa tu na zilivyo lugha nyingine kubwa kubwa Duniani.

Umashuhuri wa Think and Grow Rich unajidhihirisha na idadi ya watu waliowahi kukisoma kitabu hiki mpaka sasa, karibu watu milioni 100 pamoja na watu mbalimbali mashuhuri waliowahi kukisoma wakiwemo Marais, Mawaziri wakuu na hata Wafalme. ELON Musk, Steve Jobs, Brian Tracy, Donald Trump, Oprah Winfrey, MuhamadAlly, Nelson Mandela, Tony Robinson, Barack Obama na hata Robert Kiyosaki ni watu Mashuhuri duniani waliowahi kukiri kukisoma na kikachangia kwa kiasi kikubwa mafanikio yao kimaisha. Waulize watu wengi wanaofuatilia elimu hizi za mafanikio, wengi watakuambia katika listi ya vitabu vyao bora 10, Think and Grow Rich kama siyo namba moja basi hakikosekani katika hiyo orodha.

Wakati fulani nilipokuwa naanza kusoma vitabu mbalimbali vya mafanikio na maendeleo binafsi ya watu, karibu kila mwandishi mashuhuri niliyesoma kazi zake niligundua kuna mahali fulani alikiri kuhamasishwa na falsafa hii ya kitabu cha Napoleo Hill THINK & GROW RICH, Sasa nikajiuliza, "*ikiwa kama kila mwandishi nguli anakiri kuhamasishwa kwa namna moja ama nyingine na kitabu hiki kwanini basi moja kwa moja nisikisome*?" Baada ya kukisoma matokeo yake ndiyo haya, nikaamua kabisa kukitafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Niligundua hazina ya ajabu iliyokuwa imejificha ndani ya kurasa zake!

Kwahiyo kitu kikubwa kilichonisukuma kutafsiri kitabu hiki ni kuwarahisishia kazi ya kukisoma Watanzania na Wana Afrika Mashariki wengine kwa ujumla wanaotamani kukisoma lakini wanapata changamoto ya lugha. Si kama wote hawajui kiingereza hapana, bali watu wengi wasingelipenda kurejea-rejea kwenye kamusi wakati wa kusoma kutokana na kitabu hiki pengine kutumia kiingereza chenye msamiati mgumu kidogo kwa baadhi yao. Ni kitabu kila mpenda mafanikio hapaswi kukikosa.

***PETER AUGUSTINO TARIMO, 2021***

.

SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## MTU ALIYEFIKIRI NJIA YAKE KUWA MBIA NA THOMAS A. EDISON

UKWELI, 'FIKRA'(MAWAZO) ni vitu halisi' na ni vitu vyenye nguvu pale vinapochanganywa na nia, uvumilivu na *shauku kubwa* katika kuvigeuza kuwa utajiri ama vitu vingine vinavyoweza kushikika.

Edwin C. Barnes aligundua namna ilivyokuwa kweli kwamba, ni dhahiri watu huwa *matajiri kutokana na kufikiri.* Ugunduzi wake haukutokea mara moja, ulitokea kidogokidogo, ukianzia na *shauku kubwa* ya kuja kuwa mshirika wa kibiashara na gwiji Thomas Edison.

Moja ya tabia kubwa ya shauku ya Barnes ilikuwa kwamba ilikuwa dhahiri. Alitaka kufanya kazi *na* Edison na wala siyo *kumfanyia* kazi. Fuatilia

kwa makini maelezo ya jinsi alivyoweza kuibadilisha *shauku* yake kuwa kweli, na utakuwa na uelewa mzuri wa kanuni 13 zinazomfanya mtu kuwa tajiri.

Wakati hii shauku au msukumo wa fikra, ulipong'ara kwa mara ya kwanza ndani ya akili yake, hakuwa katika nafasi nzuri kuishughulikia, Vikwazo viwili vilimzuia. Cha kwanza, hakuwa anafahamiana na Bwana Edison, na cha pili hakuwa na fedha za kutosha kulipa nauli ya treni mpaka Orange New Jersey. Vikwazo hivi viwili vilitosha kuwakatisha tamaa wengi wa watu katika kujaribu kutekeleza shauku.

Lakini shauku yake haikuwa ya kawaida. Alikuwa ni mwenye dhamira ya dhati kutafuta njia ya kuitekeleza shauku yake kiasi kwamba mwishoni aliamua kusafiri kwa treni la mizigo kuliko kukosa kabisa kwenda.

Aliwasili mwenyewe katika maabara ya Bwana Edison na kutangaza kwamba alikuwa amefika pale kuingia ubia wa biashara na Mgunduzi. Katika mazungumzo ya mkutano wa kwanza kati yao miaka kadhaa baadaye, Bwana Edison alisema, "Alisimama pale mbele yangu, huku akitazama kama mzururaji wa kawaida, lakini kulikuwa na kitu kwenye taswira ya sura yake ambacho kilitoa tafsiri kwamba alikuwa na dhamira ya kupata kile alichokuwa amekifuata.

Nilikuwa nimejifunza kutokana na uzoefu wa miaka mingi na watu kwamba, mtu *anapotamani sana* kitu

kiasi cha kuweka rehani mustakabali wake mzima wa baadaye kwa ajili ya kukipata, bila shaka atakuwa na uhakika wa kufanikiwa kukipata. Nilimpatia fursa aliyoomba kutokana na kuona kwamba alikuwa ameifanya akili yake kusimamia mpaka amefanikisha. Matukio ya baadaye yalikuja kudhihirisha kwamba hakukuwa na kosa lililofanyika."

Kile tu alichotamka Barnes kwa Bwana Edison siku hiyo kilikuwa na umuhimu mdogo kushinda vile alivyokuwa akifikiria. Edison mwenyewe alitamka hivyo!. Isingewezakuwa ni muonekana wa kijana Barnes uliomwezesha kupata kazi katika ofisi za Edison, kwa hilo ilikuwa ni kinyume kabisa naye. Ilikuwa ni kile *alichofikiri* ndicho kilichomuwezesha. Ikiwa umuhimu wa sentesi hii ungeweza kufikishwa barabara kwa kila mtu anayeisoma, kusingelikuwa tena na umuhimu wa kusoma sehemu ya kitabu hiki iliyobakia.

Barnes hakufanikiwa kupata ubia na Edison mara tu alipohojiwa kwa mara ya kwanza. Alipata kwanza nafasi ya kufanya kazi ambayo haikuwa na umuhimu kwa Edison, lakini iliyokuwa muhimu zaidi kwa Barnes mwenyewe. Ilimpatia fursa ya kuonyesha hadharani "Bidhaa" yake ambapo "Mbia" wake aliyemkusudia angeweza kuiona.

Miezi ilipita kukiwa hakuna chochote kilichotokea dhahiri kuhusiana na lengo lililokuwa limekusudiwa na ambalo Barnes alikuwa ameliweka akilini mwake kama *lengo lake kuu*. Lakini kuna kitu muhimu

# FIKIRI NA UTAJIRIKE
## THNK & GROW RICH-SWAHILI EDITION

Kwa takriban muda wa miaka 20 Napoleon Hill alifanya utafiti na kuwahoji watu matajiri na waliokuwa na mafanikio makubwa kipindi chake wapatao 500. Miongoni mwao alikuwemo Andrew Carnegie, Henry Ford, Charles Schwab, King Gillete, Alexander Graham Bell na wengineo. Matokeo ya kazi hiyo ni kitabu hiki Mashuhuri Duniani cha Fedha na mafanikio, Fikiri na Utajirike(Think & Grow Rich)

Kitabu hiki kimethibitisha pasi na shaka kuwa mtu yeyote anaweza akafanikiwa maishani bila kujali rangi yake, kabila, jinsia, dini, umri, elimu, hali ya kifedha, au kilema kingine chochote alichonacho. “Binadamu anaweza kufanya au kuwa chochote kile atakacho, ilimradi tu kitu hicho anaweza kukifikiria akilini”. Mafanikio Napoleon amemaanisha ni kitu chochote kile unachokitaka maishani na wala siyo lazima iwe ni fedha au utajiri peke yake.

Kwa mara ya kwanza kabisa Think & Grow Rich hatimaye kimetafsiriwa katika lugha adhimu ya Kiswahili na mtu yeyote yule anaweza kujifunza Siri za mafanikio kupitia kanuni 13 zilizogunduliwa na Napoleon Hill katika mahojiano yake na watu hao mashuhuri 500.

Ni kwa njia ya kukisoma tu ndipo mtu anaweza akagundua siri ni kwanini kitabu hiki kimeweza muda wote kuendelea kubakia kuwa kitabu bora duniani miongoni mwa vitabu vingine vingi vya fedha na mafanikio ya mtu binafsi.

SELF HELP BOOKS TANZANIA

ISBN: 978-9976-88-937-6